

**Hotuba ya Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Bw. Ladislaus Mwamanga, iliyotolewa wakati wa ufunguzi wa Mafunzo kwa Wawezeshaji wa Mamlaka za maeneo utekelezaji kuhusu Maandalizi, utekelezaji na usimamizi wa Miradi ya Kutoa Ajira za Muda chini ya Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini - TASAF Awamu ya Tatu kipindi cha pili.**

- Mkurugenzi wa Mamlaka ya Eneo la utekelezaji,
- Timu ya Wawezeshaji wa Mafunzo kutoka TASAF,
- Timu ya Wawezeshaji wa Kitaifa,
- Afisa Ufuatiliaji-TASAF
- Mratibu wa Mpango,
- Washiriki wa Mafunzo,
- Wageni Waalikwa,
- Mabibi na Mabwana,

Awali ya yote nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia afya njema na kutuwezesha kukutana hapa. Aidha niwapongeze wote mliofika kuhudhuria kikao kazi hiki cha kujenga uelewa wa pamoja juu ya uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa Miradi ya Kutoa Ajira za Muda.

Hiki ni kikaokazi kinachohusu; Maandalizi ya utekelezaji na usimamizi wa Miradi ya Kutoa Ajira za Muda chini ya Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini. Kikao kazi hiki kinafanyika kwa mara ya kwanza katika eneo hili la Mamlaka ya utekelezaji katika mzunguko wa pili wa utekelezaji wa miradi kwa mwaka 2022/23.

Kama mnavyofahamu, mzunguko wa kwanza wa utekelezaji miradi unaendelea katika Mamlaka za Maeneo ya Utekelezaji 51 nchini kote. Kwa mwaka 2022/23 Mzunguko wa pili utanza katika maeneo mengine 72 na kufanya jumla ya maeneo 123 yatakayotekeleza miradi ikijumuisha Mamlaka hii ya utekelezaji.

**Ndugu Washiriki wa Mafunzo,**

Kipindi cha Pili cha Awamu ya Tatu ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF III) kilizinduliwa na Hayati Mhe. Dr. John Pombe Joseph Magufuli, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Februari 2020.

Utekelezaji wa Mpango unafanyika katika Mamlaka zote za maeneo ya utekelezaji za Tanzania Bara na Zanzibar na unatarajia kuzifikia Kaya milioni moja na laki nne na nusu zinazokadiriwa kuwa na watu zaidi ya milioni 7 kote nchini, hii ikiwa ni nyongeza ya kaya laki tatu na nusu ikilinganishwa na Kipindi cha Kwanza.

Mkazo mkubwa katika kipindi hiki cha Pili ni kuziwezesha Kaya kufanya kazi ili kujiongezea kipato kupitia utekelezaji wa Miradi ya Kutoa Ajira za Muda. Kaya zitakazoshiriki utekelezaji wa miradi hii ni zenye watu wenye uwezo wa kufanya kazi na wenye umri wa kuanzia miaka 18 hadi 65.

### **Ndugu Washiriki wa Mafunzo,**

Miradi ya Kutoa Ajira za Muda inalenga; kutoa ajira kwa kaya maskini wakati wa kipindi cha hari ili wanakaya hao;

- Wasishawishike kuuza rasilimali walizonazo kwa ajili ya kupata fedha
- Washiriki katika ujenzi wa miondombinu ya jamii
- Waweze kupokea ujira utakaowasaidia kuongeza kipato cha kaya na hivyo kupunguza umaskini.
- Wapate ujuzi kupitia miradi itakayotekelezwa.

### **Ndugu Washiriki wa Mafunzo,**

Katika kipindi cha kwanza cha Mpango wa kunusuru kaya za walengwa jumla ya miradi **9,440** ya kutoa ajira za muda ilitokelezwa katika Mamlaka ya Maeneo ya utekelezaji 44. Miradi hii ilitokelezwa kwa jumla ya gharama ya shilingi za Kitanzania Bilioni **119**, kati ya hizo Bilioni **83.3** ilitumika kwa kulipa ujira wa walengwa na shilingi za Kitanzania Bilioni **35.7** kwa ajili ya vifaa vya miradi na usimamizi.

### **Ndugu Washiriki wa Mafunzo,**

Kama nilivyotangulia kusema hapo awali, TASAF awamu ya Tatu kipindi cha pili inaendelea kutekeleza jumla ya Miradi ya Ajira za Muda 3185 katika Mamlaka ya Maeneo ya utekelezaji 51 kwa mwaka 2021/22. Katika kipindi cha 2022/23 jumla ya Mamlaka za maeneo ya utekelezaji 123 zitatekeleza miradi ya kutoa ajira za muda ikiwa ni ongezeko la Mamlaka za maeneo ya utekelezaji 72.

### **Ndugu Washiriki wa Mafunzo,**

Lengo kuu la mafunzo haya ni kujenga uwelewa wa pamoja kwa **Wawezeshaji wa Mamlaka za maeneo utekelezaji** kuhusu uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa miradi ya kutoa ajira za muda ili kutekeleza miradi yenye tija inayokidhi viwango vya kisékta na ubora unaokubalika.

Ni matumaini yangu baada ya mafunzo haya timu hii ya Wataalam wa Kisékta itakuwa imejengewa uwezo wa kutosha wa kusimamia shughuli za Miradi ya Kutoa Ajira za Muda katika ngazi ya vijiji, mitaa na shehia.

**Ndugu Washiriki wa Mafunzo,**

Ni matarajio yangu kuwa mtayapa umuhimu mkubwa mafunzo haya kwa kushiriki kikamilifu kwa siku zote sita zilizopangwa.

Baada ya maelezo haya machache, napenda nichukue fursa hii kuwatakia kikao kazi chema cha kujenga uelewa wa pamoja juu ya uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa Miradi ya Kutoa Ajira za Muda kwa **Wawezeshaji wa Mamlaka za maeneo ya utekelezaji**.

**Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.**